

REF: PPR/08- 2/11

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI ELEKEZI/KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA TAREHE 15 AGOSTI 2011

Kama ilivyo ada, na kulingana na Kanuni ya Kukokotoa bei za bidhaa za mafuta ya petroli bei zimekuwa zikikokotolewa na kutangazwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kila baada ya wiki mbili. EWURA inatangaza bei elekezi/kikomo za mafuta ya petroli nchini zitakazoanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 15 Agosti 2011**. Bei hizi zimekokotolewa kwa kuzingatia kanuni mpya iliyoanza kutumika mwanzoni mwa mwezi huu. Pamoja na kutambua bei elekezi/kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimepanda ikilinganishwa na zile zilizokuwa kwenye toleo lililopita la tarehe 03 Agosti 2011. Katika toleo hili bei zimepanda kama ifuatavyo: Petroli TZS 100.34 sawa na asilimia 5.51, Dizeli TZS 120.47, sawa na asilimia 6.30 na Mafuta ya taa TZS 100.87, sawa na asilimia 5.30. Mabadiliko haya ya bei za mafuta nchini yametokana na kupanda sana kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na kuendelea kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Kwa mfano, kwa viwango vya bei zilizotumika katika chapisho hili, bei katika soko la dunia zimepanda kwa wastani wa asilimia 5.42 na thamani ya shilingi ya Tanzania imeshuka kwa shilingi 47.12 (asilimia 2.96) kwa dola moja ya Marekani. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimepanda kama ifuatavyo: Petroli TZS 110.34 sawa na asilimia 5.70; Dizeli TZS 120.47 sawa na asilimia 6.54; na Mafuta ya Taa TZS 100.87 sawa na asilimia 5.49.
- (b) Bei za rejareja na za jumla zingepanda zaidi endapo formula ya zamani ingeendelea kutumika. Kwa kulinganisha vigezo vilivyo katika fomula ya zamani na fomula mpya, bei za mafuta zingekuwa kama ifuatavyo:

Aina ya Mafuta	Bei za Rejareja (TZS/L)		Bei za Jumla (TZS/L)	
	Kwa Formula ya zamani	Kwa Formula Mpya	Kwa Formula ya zamani	Kwa Formula Mpya
Petroli	2,298.33	2,114.12	2,230.07	2,046.62
Dizeli	2,213.36	2,031.31	2,140.80	1,963.81
Mafuta ya Taa	2,188.89	2,005.40	2,116.33	1,937.90

Kama inavyoonyesha kwenye jedwali hapo juu, formula mpya inaendelea kutoa unafuu kwa watumiaji ukilinganishwa na kama fomula ya zamani ingetumika. Ni dhahiri kuwa **vigezo viwili vikubwa vinavyochochea kupanda kwa kasi kwa bei ya mafuta nchini ni kupanda kwa bei ya mafuta kwenye**

soko la dunia na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ukilinganisha na dola ya Marekani, sarafu ambayo inatumika kuagizia mafuta hayo.

- (c) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (d) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa mwezi Julai 2011.**
- (e) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (f) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Elekezi		
	Petroli (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)	Dizeli (TZS/LT)
Dar es Salaam	2,114	2,005	2031
Arusha	2,198	2,089	2115
Arumeru	2,198	2,089	2115
Karatu	2,216	2,108	2133
Monduli	2,203	2,095	2121
Ngorongoro (Loliondo)	2,275	2,166	2192
Kibaha	2,119	2,010	2036
Bagamoyo	2,125	2,016	2042
Kisarawe	2,121	2,013	2038
Mkuranga	2,124	2,015	2041
Rufiji	2,142	2,033	2059
Dodoma	2,173	2,064	2090
Konoda	2,205	2,096	2122
Kongwa	2,170	2,061	2087

Mpwapwa	2,174	2,065	2091
Iringa	2,178	2,069	2095
Kilolo	2,183	2,074	2100
Ludewa	2,244	2,135	2161
Makete	2,237	2,128	2154
Mufindi	2,188	2,079	2105
Njombe	2,206	2,098	2124
Bukoba	2,329	2,220	2246
Biharamulo	2,303	2,194	2220
Karagwe	2,345	2,236	2262
Muleba	2,320	2,211	2237
Ngara	2,261	2,153	2178
Misenyi	2,337	2,228	2254
Kigoma	2,345	2,236	2262
Kasulu	2,331	2,222	2248
Kibondo	2,309	2,200	2226
Moshi	2,188	2,079	2105
Hai	2,191	2,082	2108
Mwanga	2,181	2,072	2098
Rombo	2,209	2,100	2126
Same	2,174	2,065	2091
Siha	2,194	2,085	2111
Lindi	2,173	2,064	2090
Kilwa Masoko	2,148	2,039	2065
Liwale	2,194	2,085	2111
Nachingwea	2,202	2,093	2119
Ruangwa	2,200	2,091	2117
Babati	2,236	2,127	2153
Hanang	2,247	2,138	2164
Kiteto	2,247	2,139	2164
Mbulu	2,249	2,140	2166
Simanjiro	2,268	2,159	2185
Musoma	2,292	2,184	2209
Bunda	2,283	2,175	2201
Serengeti	2,338	2,229	2255
Tarime	2,303	2,195	2220
Mbeya	2,221	2,112	2138
Chunya	2,230	2,122	2148
Ileje	2,234	2,125	2151
Kyela	2,237	2,128	2154
Mbarali	2,205	2,096	2122
Mbozi	2,230	2,121	2147
Rungwe	2,230	2,121	2147

Morogoro	2,139	2,030	2056
Mikumi	2,155	2,046	2072
Kilombero	2,177	2,068	2094
Mahenge	2,187	2,078	2104
Kilosa	2,157	2,048	2074
Mvomero	2,149	2,040	2066
Mtwara	2,186	2,078	2104
Masasi	2,212	2,103	2129
Newala	2,218	2,109	2135
Tandahimba	2,211	2,102	2128
Mwanza	2,264	2,155	2181
Geita	2,305	2,196	2222
Kwimba	2,300	2,191	2217
Magu	2,272	2,163	2189
Misungwi	2,269	2,161	2187
Sengerema	2,296	2,187	2213
Ukerewe	2,323	2,214	2240
Sumbawanga	2,287	2,178	2204
Mpanda	2,321	2,212	2238
Nkasi	2,300	2,191	2217
Songea	2,237	2,129	2154
Mbinga	2,271	2,162	2188
Namtumbo	2,266	2,157	2183
Tunduru	2,296	2,187	2213
Shinyanga	2,243	2,134	2160
Kahama	2,256	2,148	2174
Bukombe	2,269	2,160	2186
Bariadi	2,284	2,175	2201
Kishapu	2,271	2,162	2188
Maswa	2,275	2,166	2192
Meatu	2,282	2,173	2199
Singida	2,205	2,096	2122
Iramba	2,217	2,108	2134
Manyoni	2,189	2,080	2106
Tabora	2,268	2,159	2185
Igunga	2,222	2,113	2139
Nzega	2,233	2,124	2150
Sikonge	2,280	2,171	2197
Urambo	2,281	2,172	2198
Tanga	2,160	2,051	2077
Handeni	2,151	2,042	2068
Kilindi	2,174	2,065	2091
Korogwe	2,153	2,044	2070

Lushoto	2,163	2,054	2080
Mkinga	2,174	2,065	2091
Muheza	2,160	2,051	2077
Pangani	2,167	2,058	2084

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	2,046.62	1,963.81	1,937.90



Haruna Masebu
MKURUGENZI MTENDAJI
EWURA